NISHATI
HABARI ZA NISHATI
News Bulletin
www.nishati.go.tz | Wizara ya Nishati | wizara_ya_nishati_tanzania | @Nishati2017 | Wizara ya Nishati

Toleo Namba 45 | Desemba 1 - 31, 2022

# RAIS SAMIA ATOA MWAKA MMOJA KWA TAASISI KUPIKIA NISHATI SAFI




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akifungua Kongamano la Kitaifa la Nishati Safi ya Kupikia Novemba 01, 2022 katika ukumbi wa JNICC.*

**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
**Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma**




# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
**Mhandisi Felchesmi Mramba**
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**

Lucas Gordon

**Wasiliana nasi kwa simu namba** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148
au

**Fika Ofisi ya Mawasiliano**
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma





*www.nishati.go.tz*
*Wizara ya Nishati*
*@Nishati2017*
*wizara_ya_nishati_tanzania*
*Wizara ya Nishati*



*Viongozi mbalimbali pamoja na Wananchi wakiwa kwenye Kongamano la Kitaifa kuhusu Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Novemba 01, 2022.*

# RAIS SAMIA ATOA MWAKA MMOJA KWA TAASISI KUPIKIA NISHATI SAFI

**Na Timotheo Mathayo, Dar es salaam.**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameagiza Taasisi/Idara za umma na binafsi zenye watu wasiopungua 300 kutumia nishati safi kupikia badala ya kutumia kuni au mkaa ambazo zinaleta madhara ya kiafya pamoja na uharibifu wa mazingira.

Alitoa agizo hilo Novemba 01, 2022 wakati wa ufunguzi wa mjadala kuhusu Nishati Safi ya Kupikia uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa wa Julius Nyerere.

Alimuagiza Waziri wa Nishati, January Makamba kuhakikisha Idara na Taasisi zote za umma na binafsi zenye mkusanyiko wa watu zaidi ya 300 zinatumia nishati safi kupika chakula.

"Hili agizo nataka lianze kutekelezwa mwaka 2023/2024. Mwaka huu wote wa 2022/2023 utumike kwa maandalizi ili Shule, Magereza, Majeshi na taasisi nyingine zenye watu wengi zaidi wapike kwa kitumia nishati safi." Alisema Rais Samia.

Awali akimkaribisha Rais Samia kufungua mjadala huo, Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba alisema kupika sio adhabu, hivyo sio vizuri watu kupika huku wakitokwa machozi kutokana na moshi wa kuni au mkaa.

Alisema kuwa watoto wa kike wapo katika hatari ya mbalimbali kutokana na wao kwenda porini kutafuta kuni za kupikia au kuuza ili wapate kipato cha kaya.

Alisema kuwa, lengo la mjadala huo ni kutaka jamii iondokane na matumizi ya nishati isiyo salama, kwa kuwa nishati hiyo ina athari kwa afya ya binadamu, lakini pia inachangia mabadiliko ya tabia nchi na pia imeelekezwa kufikia asilimia 80% ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2032.

# SERIKALI KUUNDA KIKUNDI KAZI KUHUSU NISHATI YA KUPIKIA

**Na Timotheo Mathayo, Dar es Salaam.**

Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza Wizara ya Nishati kuunda kikundi kazi kwa ajili ya kupitia na kuchakata Sera zilizopo kwa ajili ya kuelekea kwenye mpango wa taifa kuondokana na matumizi ya gesi chafu ya kupikia ifikapo 2032.

Alitoa agizo hilo Jumanne, Novemba 01, 2022 alipokuwa akifungua mjadala wa kitaifa kuhusu matumizi ya Nishati safi ya kupikia uliofanyika katika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es salaam.

Kikundi kazi hicho kitaongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Nishati itaratibu na kufanya shughuli za sekretarieti za kikundi hicho.

Ili kuongeza tija na ufanisi Rais Samia aliagiza muundo wa kikundi kazi ujumuishe pamoja wataalam kutoka Idara na Taasisi za umma, pia wawepo watu kutoka sekta binafsi na wadau




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan (wa tatu kushoto) na Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba ( wa nne kulia ) wakiwa na viongozi mbalimbali pamoja na Wananchi wakati wa Kongamano la Kitaifa kuhusu Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar Es Salaam, Novemba 01, 2022.*



*Viongozi mbalimbali pamoja na Wananchi wakiwa kwenye Kongamano la Kitaifa kuhusu Nishati Safi ya Kupikia lililofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, Novemba 01, 2022.*

# SERIKALI KUUNDA KIKUNDI KAZI KUHUSU NISHATI YA KUPIKIA

wengine wa mazingira.

"Kikundi kazi kikapitie Sera na miongozo mbalimbali ili kije na mpango mkakati na dira ya miaka kumi kikielekeza mambo muhimu ya kufanya ili ifikapo 2032 kila mtu atumie nishati safi ya kupikia," amesema Rais Samia.

Alisema kuwa matumizi ya nishati safi ya kupikia yatasaidia wanawake kuondokana na adha ya kutafuta kuni porini ambapo wengi wao wapo kwenye hatari ya kufanyiwa vitendo vya ukatili ikiwemo kushambuliwa wanyama wakali na nyoka.

Pia muda wanaoupoteza porini kutafuta kuni wautumie kwa kufanya shughuli za uzalishaji mali kama kufuma na kufanya biashara ndogo ndogo.

Aliahidi kuwa serikali katika bajeti ya mwaka 2023/2024 itatenga fedha kwa ajili ya kuanzisha mfuko wa nishati safi ya kupikia utakaoshughulikia masuala ya utafiti na uwekezaji katika kutatua changamoto zilizopo.

Rais Samia alisema takwimu zinaonyesha kuwa kaya zinazotumia gesi kupikia ni 5% na zinazotumia umeme ni 3% nchini Tanzania.

Dr. Paulina Chale kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili alisema kuwa idadi ya watu wanaougua magonjwa ya mfumo wa hewa ni kubwa yakiwemo yanayosababishwa na matumizi ya kuni na mkaa kwa muda mrefu.

Waziri wa Nishati, January Makamba alisema atasimamia na kutekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Rais ili kutimiza lengo la serikali ifikapo mwaka 2032 kila kaya wapike kwa kutumia Nishati safi.

# WIZARA YA NISHATI YAANZA KUTEKELEZA MAAGIZO YA RAIS

**Na Timotheo Mathayo, Dar es salaam.**

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amesema kuwa Wizara ya Nishati imeanza utekelezaji wa agizo la Rais alilolitoa wakati wa ufunguzi wa Mjadala wa Nishati Safi ya Kupikia ambapo aliagiza taasisi zote za umma na binafsi zenye watu zaidi ya 300 kupika kwa kutumia nishati safi.

Makamba alitoa kauli hiyo Novemba 03, 2022 wakati alipokuwa anafunga mjadala kuhusu Nishati safi ya kupikia uliofanyika ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere, Dar es salaam.

Kufuatia agizo hilo lililotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Makamba alisema kuwa amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati ashirikiane na Wizara nyingine waweze kuorodhesha taasisi zilizo chini yao zenye watu zaidi ya 300 kwa ajili ya kuanza matumizi ya Nishati safi ya kupikia.

Alisema Serikali na wadau wengine wapo katika mchakato wa kusambaza mitungi ya gesi kila eneo nchini ili iwe rahisi kuwafikia wananchi.

"Serikali imetoa Sh.Bilioni 6 kwa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) ili waendelee na kazi za kusafirisha na kusambaza gesi kutoka Mtwara." Alisema Makamba

WaziriMakamba alitoa wito kwa wawekezaji na wasambazaji wa gesi majumbani kujitokeza na kufanya kazi hiyo ili lengo la Serikali litimie haraka.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mha.Hassan Seif Said ameahidi kwamba watashirikiana na TPDC kusambaza nishati safi ya kupikia ili iwafikie wakazi wengi wanaoishi katika maeneo ya vijijini.



# UCHIMBAJI GESI KITALU CHA RUVUMA UKAMILIKE KWA WAKATI - MAKAMBA

Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba, ameliagiza Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuhakikisha mradi wa uchimbaji wa gesi kitalu cha Ruvuma kilichopo mkoani Mtwara unakamilika kwa wakati.

Mhe. Makamba aliyasema hayo tarehe 25/11/2022 jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya uwekaji saini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara kati ya Wizara ya Nishati, TPDC, Kampuni ya ARA Petroleum na Kampuni ya Ndovu Resources.

"Dhamira ya Serikali ni kuona mradi huo unakamilika ndani ya miezi 12 hadi 18 na hatutegemei kusikia mradi huo unachelewa kutokana na changamoto ya fedha.Mradi huo ukikamilika utakuwa mradi wa kwanza wa gesi ambao utalinufaisha Taifa katika nyanja mbalimbali ikiwemo Serikali kupata Mrabaha (12.5%) , kupata kodi, Serikali kupata gawio la mapato yatokanayo na mauzo ya gesi pia ajira kwa wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara." Alisema Mhe. Makamba.




*Hafla ya uwekaji saini Mkataba wa Nyongeza wa Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (PSA) Kitalu cha Ruvuma-Mtwara baina ya Wizara ya Nishati, TPDC, Kampuni ya ARA Petroleum na Kampuni ya Ndovu Resources. (Wa Tatu kushoto) ni Waziri wa Nishati, Mhe.January Makamba na wa Pili kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.*

Waziri Makamba aliongeza kuwa, "pia eneo la Lindi, Serikali imeamua kujenga Chuo (Polytechnic) cha Masuala ya Mafuta, Gesi na Umeme, ili kujengea watu wetu uwezo, lakini pia tutajenga Special Economic Zone ndani ya eneo la mradi ili kuchochea maendeleo ya Lindi na Mtwara baada ya mradi kukamilika."

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alisema utafiti na ugunduzi wa gesi ulishafanyika na kinachofanyika sasa hivi ni kuanza kwa ujenzi wa bomba la gesi kutoka eneo la Ntorya hadi Madimba na baada ya kukamilika kwa ujenzi huo uzalishaji wa gesi utaanza.

Dkt. Mataragio alisema kuwa, uwekezaji huo wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 500 unatarajiwa kuzalisha takribani futi za ujazo trilioni 1.6 ambacho ni kiasi cha gesi kilichogunduliwa katika eneo hilo na kuweka wazi kuwa utekelezaji wake utasaidia kuongeza chachu na wawekezaji wengi zaidi.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya ARA Petroleum (Tanzania), Ndg. Erhan Saygi aliishukuru Serikali ya Tanzania hususan viongozi wa Serikali za Vijiji kwa ushirikiano walioonyesha na kuongeza kuwa, kukamilika kwa mradi kutachagiza uboreshaji wa miundombinu na kuongeza ajira ili kukuza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na vongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Lindi Bi. Zainab Telack, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Kanali Ahmed Abbas Ahmed pamoja na Wabunge wa Mikoa ya Lindi na Mtwara.

# BYABATO AWATAKA WANANCHI MBARALI KUTOINGIZA MIFUGO KWENYE VYANZO VYA MAJI



*Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula (wa tatu kulia) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kuwasili Mbarali mkoani Mbeya kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya Matumizi ya ardhi. Katikati ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*




*Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula, wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera walipokwenda kutazama na kujionea hali halisi ya upungufu wa maji katika mto Ruaha Mkuu.*

**Na Godfrey Mwemezi, Mbeya.**

Naibu waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amewataka wananchi wa Kata ya Ubaruku Mbarali mkoani Mbeya kutoingiza mifugo kwenye vyanzo vya maji badala yake wavitunze ili visaidie katika upatikanaji wa nishati ya umeme nchini.

Byabato aliyasema hayo tarehe 25 Oktoba, 2022 katika mkutano wa hadhara na wananchi wa eneo la Ubaruku, Mbarali wakati Kamati

# BYABATO AWATAKA WANANCHI MBARALI KUTOINGIZA MIFUGO KWENYE VYANZO VYA MAJI



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byababto akizungumza na wananchi wa Kata ya Ubaruku wakati Kamati ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta walipofanya ziara kwenye eneo la Mto Ruaha Mkuu mkoani Mbeya.*

ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta walipofanya ziara kwenye eneo la Mto Ruaha Mkuu ambapo Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imetangaza kwamba vijiji vitano na vitongoji 41 na sehemu ndogo ya kitongoji cha Magwalisi ambacho kipo kwenye Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa wilayani Mbarali wananchi wanatakiwa kuhamishwa ili kupisha hifadhi.

Lengo la uamuzi huo wa Serikali ni kutunza na kulinda ardhi oevu na vyanzo vya kupokea na kutunza maji yanayotiririka kutoka mito mbalimbali.

Byabato alisema kuwa, Mto Ruaha ni moja ya mito inayotegemewa kupeleka maji katika bwawa la Mtera na Bwawa la Julius Nyerere hivyo ni vyema ukatunzwa na kuhifadhiwa kwa maslahi mapana ya nchi.

"Tunakubaliana kuwa shughuli zote zinatuhusu sisi wenyewe na sisi Wizara ya Nishati tunayategemea maji hayohayo kuweza kuzalisha umeme, na umeme ukishazalishwa tunautumia kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kwenye viwanda vyetu vinavyochakata mazao mbalimbali hivyo, wanambarali tutunze vyanzo vyetu vya maji". Alisema Byabato

# ULETAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA UNA TIJA - PAC



*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) wakiwa katika eneo la gati ya kushushia mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam mara baada ya kufika bandarini hapo kukagua miundombinu ushushaji na upimaji mafuta.*

**Na Mwandishi Wetu**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeeleza kuwa, kazi ya uletaji wa mafuta kwa pamoja nchini inayosimamiwa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) ina tija kwa Taifa kutokana na sababu mbalimbali ikwemo ya nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta ikiwemo dizeli na petroli.

Hayo yalisemwa na Wajumbe wa Kamati hiyo baada ya kukagua miundombinu ya kushusha na kupima mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na hifadhi kubwa ya mafuta ya kampuni ya TIPER ambayo Serikali ni mbia kwa umiliki wa hisa asilimia 50.

Ziara hiyo iliyoongozwa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato pamoja na Naibu Katibu Mkuu, Kheri Mahimbali ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Eng.Felchesmi Mramba, ilifanyika tarehe 14 Novemba, 2022, ambapo Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Japhet Hasunga alisema kuwa, lengo la ziara lilikuwa ni kuona uwezo wa miundombinu hiyo katika kushusha na kuhifadhi mafuta.

Mhe. Hasunga alieleza kuwa, baada ya ukaguzi huo Kamati hiyo imejihakikishia kwamba miundombinu iliyopo ya ushushaji na uhifadhi mafuta ina uwezo wa kukidhi mahitaj ya nchi hivyo Kamati hiyo imefurahishwa na uwepo wa miundombinu hiyo.

Hata hivyo, Kamati hiyo ilitoa wito kwa TIPER kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta katika maeneo mengine ya nchi ili kuongeza uwezo wa kampuni na



*Baadhi ya miundombinu ya kushusha mafuta kutoka kwenye Meli katika Bandari ya Dar es Salaam.*



*Moja ya tenki la kuhifadhi mafuta la kampuni ya TIPER jijini Dar es Salaam.*

# ULETAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA UNA TIJA - PAC




*Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) wakiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara ya Nishati, watendaji wa Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA), Bandari ya Dar es Salaam na TIPER mara baada ya kukagua miundombinu ya kuhifadhi mafuta ya kampuni ya TIPER jijini Dar es Salaam.*

nchi katika kuhifadhi mafuta na pia kuleta urahisi katika usafirishaji wa mafuta hayo ndani na nje ya nchi.

Awali, kabla ya kufanyika kwa ziara hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PBPA, Erasto Mulokozi, aliieleza Kamati hiyo kuwa, kutoka Wakala huo uanzishwe mwaka 2015 umekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji na yenye viwango vya ubora unaohitajika.

Manufaa mengine ni Serikali kuweza kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia takwimu sahihi, kuweza kupanga bei elekezi ya mafuta pamoja na kupata unafuu wa gharama za uletaji wa mafuta nchini kutokana na uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa wastani wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 200 Sawa na shilingi bilioni 462 huokolewa kwa mwaka.

Aidha alisema kuwa, kutokana na mfumo huo kuleta ufanisi, nchi za jirani pia zinatumia mfumo huo kuagiza mafuta kupitia Tanzania hivyo kuipatia Serikali mapato kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya bandari.

Aliongeza kuwa, mfumo huo umesaidia kupunguza upotevu wa mafuta wakati wa kupakua mafuta kutoka melini ambapo wastani wa Tani 1100 ( lita 1,300,000) huokolewa kila mwezi sawa na shilingi bilioni 4.3.



*Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Mhe. Japhet Hasunga akizungumza jambo mara baada ya Kamati hiyo kukagua miundombinu ya kushusha mafuta kutoka kwenye Meli katika Bandari ya Dar es Salaam. Wa kwanza kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mhe.Naghenjwa Kaboyoka na wa Nne kushoto ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



*Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati , Kheri Mahimbali ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba, katika ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kukagua miundombinu ya mafuta jijini Dar es Salaam, akizungumza jambo mara baada ya kufika kwenye gati ya kushushia mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.*

# WAZIRI MAKAMBA AFUNGUA BARAZA LA WAFANYAKAZI WIZARA YA NISHATI

**Na Timotheo Mathayo, Singida.**




*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu kutoka Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa (kushoto) akiwa na Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Wizara ya Nishati, Bw. Zghambo Chinula wakiimba wimbo wa kudumisha mshikamano wa Wafanyakazi kwenye Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika mjini Singida, Novemba 25 na 26, 2022.*

Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amefungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati ambapo amewaagiza Watumishi wa Wizara kutekeleza majukumu yao kwa ubunifu, umakini, usahihi na kwa weledi kwa kuwa wanahudumu katika Wizara inayosimamia sekta muhimu katika uchumi wa Taifa.

Makamba alitoa maagizo hayo mkoani Singida katika kikao hicho kilichofanyika Novemba 25 na 26, 2022, kwa lengo la kujadili masuala muhimu yanayohusu Wizara ya Nishati na Taasisi zilizo chini yake.

"Wizara ya Nishati imebeba uchumi wa nchi, inasimamia Mafuta, Umeme pamoja na Gesi ambavyo ni ndio vyanzo vikuu katika kutekeleza shughuli za uchumi na maendeleo ya nchi hivyo watumishi wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa uwanda mpana kwa kuzingatia umuhimu wa sekta husika." Alisisitiza Makamba

Aliwataka Watumishi pia kusimamia miiko na maadili ya kazi wanapotekeleza majukumu yao, kwa kuwa Sekta ya Nishati ina ushawishi mkubwa katika kutekeleza vitendo vya rushwa kutokana na miradi mikubwa inayotekelezwa na maadili yatakapofuatwa yataongeza uaminifu kutoka kwa wadau pamoja na wananchi



*Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Wizara ya Nishati, wakiimba wimbo maalum wa kudumisha mshikamano wa wafanyakazi katika eneo la kazi, wakati wa ufunguzi wa Mkutano, uliofanyika mkoani Singida, Novemba 25, 2022.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Wizara ya Nishati wakifuatilia hotuba ya Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba aliyoitoa kwa njia ya mtandao mkoani Singida, Novemba 25, 2022.*

# WAZIRI MAKAMBA AFUNGUA BARAZA LA WAFANYAKAZI WIZARA YA NISHATI



*Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Wizara ya Nishati, wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya hotuba ya ufunguzi wa mkutano wa Baraza hilo uliofanyika mkoani Singida, Novemba 25 na 26,2022.*

wanaopata huduma.

Waziri Makamba alisema kuwa, Wizara inaendelea na usimamizi wa miradi mbalimbali inayohusu Sekta ya Nishati ukiwemo mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) ambao umefikia asilimia 77.

Alisema kuwa, Wizara imefanikisha masuala mbalimbali na kuendelea na utekelezaji wa kazi mbalimbali ikiwemo kusambaza umeme vijijini, imefanikisha kubadilisha deni la TANESCO kuwa mtaji pamoja na la TPDC, imefikisha gridi ya Taifa mkoani Kigoma, kufanikisha upatikanaji wa fedha za kutekeleza mradi wa kuzalisha umeme wa Kakono na miradi mingine ya kimkakati.

Awali, akimkaribisha Waziri, Mwenyekiti wa kikao hicho, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba alimpongeza Waziri kwa kuleta chachu na kubuni miradi ya Sekta ya Nishati ukiwemo uliozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan wa Nishati Safi na Salama ya Kupikia.

Pia aliwapongeza watumishi wa Wizara hiyo kuwa wepesi katika kutekeleza maagizo na majukumu wanayopewa wakati wote, na amewataka kuendelea kufanya kazi kwa upendo na mshikamano.

Katibu Mkuu, alimhakikishia Waziri wa Nishati kuwa, Watumishi wataendelea kufanya kazi kwa weledi kwa kufuata kanuni, taratibu na miongozo ili kuhakikisha Wizara inaendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza Pato la Taifa.





*Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi kutoka Wizara ya Nishati wakifuatilia hotuba ya Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba aliyoitoa kwa njia ya mtandao mkoani Singida, Novemba 25, 2022.*

# WATUMISHI WATAKIWA KUJIANDAA MAPEMA KABLA YA UTUMISHI KUFIKA KIKOMO



*Mwenyekiti wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati, Mha.Felchesmi Mramba ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, akiongoza kikao hicho, kilichofanyika katika Ukumbi wa Ofisi Mkuu wa Mkoa wa Singida, Novemba 26, 2022.*

**Na.Timotheo Mathayo-Singida**

Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mha. Felchesmi Mramba amewataka Watumishi kufanya maandalizi ya kustaafu mapema wakiwa bado wapo kazini ili kuendelea kuwa na maisha bora pindi utumishi wao unapofika kikomo.

Mramba alitoa kauli hiyo mkoani Singida wakati akifunga kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Novemba 25 na 26, 2022, kwa lengo la kujadili masuala muhimu yanayohusu Wizara ya Nishati, Watumishi pamoja na Taasisi zilizo chini yake.

Mhandisi Mramba alisema kuwa, Watumishi watumie fursa mbambali wanazozipata pindi wawapo kazini ili kuendelea kujiandaa na maisha baada ya utumishi wao kufika kikomo ikiwemo kujenga nyumba za kuishi na kubuni shughuli mbalimbali za ujasiriamali ili kujiongezea kipato nje ya utumishi wa umma jambo ambalo litawasaidia hata baada ya kustaafu.

Hata hivyo, Katibu Mkuu alisema kuwa, katika kikao hicho cha siku mbili, Watumishi wameagizwa na Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Nishati Mhe. January Makamba, kutekeleza majukumu yao kwa ubunifu, umakini, usahihi na kwa weledi kwa kuwa wanahudumu katika Wizara inayosimamia sekta muhimu katika uchumi wa Taifa.

Kwa upande wa Miradi inayosimamiwa na Wizara, alisema kuwa, mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP umefikia asilimia 77 ya utekelezaji na mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka nchini Uganda hadi Tanzania pia unaendelea vizuri pamoja na miradi mingine ya kimkakati ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo.

Vilevile, alisema kuwa, katika Mkoa wa Singida, Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali ili kuhakikisha kuwa vyanzo vya umeme vilivyopo Mkoa huo vinazalisha umeme ambao utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa, vyanzo vya umeme vilivyopo ni chanzo cha umeme utakanao na upepo pamoja na ule wa jua ambao unategemea kuzalisha



*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu kutoka Wizara ya Nishati, Bi. Ziana Mlawa akiwasilisha mada ya taarifa zakiutumishi wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika mjini Singida, Novemba 26, 2022.*

# WATUMISHI WATAKIWA KUJIANDAA MAPEMA KABLA YA UTUMISHI KUFIKA KIKOMO



*Mratibu wa Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Mha. Christopher Bitesigirwe kutoka Wizara ya Nishati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati, kilichofanyika mkoani Singida, Novemba 26, 2022.*



*Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya Rasilimaliwatu Bi. Bahati C. Mtono kutoka Wizara ya Nishati, akiwasilisha Rasimu ya Waraka wa Maendeleo ya Utumishi ya Kada chini ya Wizara ya Nishati, wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Singida, Novemba 26, 2022.*

megawati 100.

Mwenyekiti wa TUGHE, Wizara ya Nishati, Zghambo Chinula alisema kuwa, changamoto zote zilizowasilishwa na Watumishi kwenye kikao cha Baraza la wafanyakazi, zimepatiwa majibu stahiki na watumishi wameahidi kuendelea kufanya kazi kwa bidii na weledi ili kufanikisha kauli mbiu isemayo "Kazi iendelee".





*Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati, wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa kikao hicho kilichofanyika mkoani Singida, Novemba 25 na 26, 2022 (Picha ya chini Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Nishati, Dorina G. Makaya.*



*Baadhi ya Wajumbe wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Nishati, wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa wakati wa kikao hicho kilichofanyika mkoani Singida, Novemba 25 na 26, 2022 (Katikati ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Wizara ya Nishati, Dorina G. Makaya.*

# TANZANIA MWENYEJI KONGAMANO LA 10 LA JOTOARDHI MWAKA 2024

Tanzania itakuwa mwenyeji wa Kongamano la 10 la Jotoardhi la Nchi za Ukanda wa Mashariki ya Afrika (African Rift Geothermal Conference - ARGeo) litakakofanyika Mwaka 2024.

Hayo yalielezwa katika Kongamano la 9 la Jotoardhi la Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati lililofanyika tarehe 3 hadi 5 Novemba, 2022 katika Mji wa Heron nchini Djibouti ambalo lilijadili uendelezaji wa nishati ya Jotoardhi katika kuzalisha umeme na matumizi mengine.

Akimwakilisha Waziri wa Nishati kwenye Kongamano hilo, Kamishna Msaidizi wa Umeme Mha. Innocent Luoga alisema "tupo tayari kuwa wenyeji wa Kongamano la 10 la Jotoardhi litakalofanyika Mwaka 2024 ili tuweze kupata manufaa ya kongamano hilo ikiwa pamoja na kuharakisha kupata umeme unaotokana na Jotoardhi."

Mhandisi Luoga alieleza kuwa, pamoja na kuimarisha ushirikiano na nchi wanachama, Tanzania itanufaika na kongamano hilo kwa kuhamasisha uendelezaji wa Jotoardhi nchini, kupata fedha za kutekeleza miradi ya Jotoardhi, pamoja na kubadilishana uzoefu na nchi zilizofanikiwa katika kuzalisha umeme kwa kutumia Jotoardhi zikiwemo Kenya na Ethiopia.




*Kamishna Msaidizi wa Umeme, Wizara ya Nishati, Mha. Innocent Luoga akitoa taarifa ya Tanzania kukubali kuwa Mwenyeji wa Kongamano la 10 la Jotoardhi kwa Nchi za Ukanda wa Afrika katika Kongamano lililofanyika tarehe 3 hadi 5 Novemba, 2022 katika Mji wa Heron, nchini Djibouti.*

Katika Kongamano hilo, Wizara ya Nishati pamoja na Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) zilipata fursa za kufanya vikao na Mashirika mbalimbali yanayofadhili miradi ya Jotoardhi ili kupata fedha za kutekeleza miradi hiyo. Mashirika hayo ni pamoja na

# TANZANIA MWENYEJI KONGAMANO LA 10 LA JOTOARDHI MWAKA 2024

**Wizara ya Nishati pamoja na Kampuni ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC) zilipata fursa za kufanya vikao na Mashirika mbalimbali yanayofadhili miradi ya Jotoardhi ili kupata fedha za kutekeleza miradi hiyo.**

Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), Mfuko wa Kuzuia Athari za Jotoardhi (GRMF) na Benki ya Maendeleo ya Biashara ya Afrika (TDB).

Kamishna Luoga aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya kuendeleza Jotoardhi nchini (TGDC) Prof. Shubi Kaijage, Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC, Mha. Mathew Mwangomba, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TGDC Mha. Shakiru Kajugus pamoja na Mjumbe wa Kamati ya ARGeo Mha. Kato Kabaka.



*Kamishna Msaidizi wa Umeme, Wizara ya Nishati, Mha. Innocent Luoga, akizungumza wakati wa Kongamano la 10 la Jotoardhi kwa Nchi za Ukanda wa Afrika lililofanyika tarehe 3 hadi 5 Novemba, 2022 katika Mji wa Heron, nchini Djibouti.*



*Ujumbe wa Tanzania uliohudhuria Kongamano la 9 la Jotoardhi la Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati lililofanyika katika Mji wa Heron nchini Djibouti. Kutoka kushoto ni Mha Kato Kabaka (Mjumbe wa Kamati ya ARGeo), Mha. Mathew Mwangomba (Kaimu Meneja Mkuu wa TGDC), Mha. Innocent Luoga (Kamishna Msaidizi wa Umeme), Prof. Shubi Kaijage (Mwenyekiti wa Bodi ya TGDC) na Mha. Shakiru Idrisa, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TGDC).*

# MAENEO YENYE UZALISHAJI YAPEWE KIPAUMBELE CHA UMEME - BYABATO



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan akizungumza na Wananchi wa Jiji la Arusha, wakati wa ziara yake mkoani humo, Novemba 23, 2022.*



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato(Mb) akizungumza na Wakazi wa Jiji la Arusha, wakati wa ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Novemba 23, 2022.*

**Godfrey Lilunga - Arusha.**

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ameliagiza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuyapatia kipaumbele cha umeme maeneo yenye shughuli za uzalishaji ili kutoathiri shughuli zao.

Byabato alitoa agizo hilo Novemba 23,2022 akiwa jijini Arusha, wakati akizungumza na wananchi kwenye ziara ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Alisema kuwa, ili kuweza kuyabaini maeneo yote yenye shughuli za uzalishaji, TANESCO washirikiane na Mamlaka za Serikali za Mitaa na baada ya kubaini maeneo hayo wayapatie kipaumbele katika kipindi hiki.

Alieleza kuwa, katika umeme unaozalishwa nchini, asilimia 60 hadi 70, unatokana na chanzo cha Gesi Asilia na asilimia 30 unatokana na maji.

Aliongeza kuwa, mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakapokamilika utaondoa changamoto ya upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini kwani jumla ya megawati 2115 zinategemewa kuzalishwa kutokana na mradi huo wa JNHPP.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato (wa pili toka kushoto) akisikiliza maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara ya Rais katika Jiji la Arusha, Novemba 23, 2022.*

# KAMATI YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI YAPATA ELIMU YA UAGIZAJI WA MAFUTA KWA PAMOJA



*Mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka akizungumza wakati wa Semina ya Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Mfumo wa Uagizaji wa mafuta kwa Pamoja nchini katika ukumbi wa Wizara ya Nishati, jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*

**Na Ruben Richard - Dodoma.**

Wajumbe wa Kamati Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) wamepata elimu kuhusu shughuli za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja zinazosimamiwa na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alisema kuwa lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwawezesha Wajumbe hao kufahamu kwa kina kuhusu utendaji wa Taasisi ya PBPA iliyopewa jukumu la kusimamia shughuli za uagizaji wa mafuta kwa pamoja.

Semina hiyo ilifanyika jijini Dodoma tarehe 6 Novemba, 2022 na kuhudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali na watendaji mbalimbali kutoka Wizara ya Nishati na Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA).

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PBPA, Erasto Mulokozi, aliieleza Kamati hiyo kuhusu historia ya shughuli za uagizaji wa mafuta nchini pia kazi zinazofanywa na taasisi hiyo kwa sasa za uagizaji na upokeaji wa mafuta.

Alisema kuwa, kutoka Wakala huo uanzishwe mwaka 2015 umekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo nchi kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji na yenye viwango vya ubora unaohitajika.

Manufaa mengine ni Serikali kuweza kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia takwimu sahihi, kuweza kupanga bei elekezi ya mafuta pamoja na kupata unafuu wa gharama za uletaji wa mafuta nchini kutokana na uagizaji wa mafuta kwa pamoja kwa wastani wa zaidi ya Dola za Marekani milioni 200 Sawa na shilingi bilioni 462 huokolewa kwa mwaka.

Aidha, alisema kuwa, kutokana na mfumo huo kuleta ufanisi, nchi za jirani pia zinatumia mfumo huo kuagiza mafuta kupitia Tanzania hivyo kuipatia Serikali mapato kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya Bandari.

Aliongeza kuwa, mfumo huo umesaidia kupunguza upotevu wa mafuta wakati wa kupakua mafuta kutoka melini ambapo wastani wa Tani 1100 ( lita 1,300,000) huokolewa kila mwezi sawa na shilingi bilioni 4.3.

Wajumbe wa Kamati hiyo walipongeza kuhusu mfumo ambao umeonesha ufanisi, ambapo pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka aliishukuru Wizara ya Nishati kupitia PBPA kwa kupata uelewa huo ambao umesaidia Kamati kufahamu Sekta pamoja na changamoto zake.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali alitoa wito kwa Wajumbe wa Kamati hiyo kuendelea kutoa ushauri na maelekezo ambayo yataiwezesha Sekta ya Nishati kuendelea kuendeshwa kwa ufanisi.

**JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**











*Fika Ofisi ya Mawasiliano,*
**Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au**
Wasiliana nasikwa **simu namba:** +255-26-2322018
**Nukushi:** +255-26-2320148

*Wizara ya Nishati* *@nishati2017* *Wizara_ya_nishati_tanzania* *www.nishati.go.tz*